TANGAZO LA SERIKALI NA. 502 la tarehe 21/7/2023

SHERIA YA USAFIRI MAJINI,
(SURA YA 165)

# KANUNI

*(Zimetengenezwa chini ya kifungu cha 222)*

## KANUNI ZA MASHARTI YA MATENGENEZO, UCHUNGUZI WA KINA, MAJARIBIO YA UENDESHAJI, MAREKEBISHO NA UKARABATI WA BOTI ZA UOKOZI WA MAISHA, VIFAA VYA UOKOZI NA VIFAA VYA KUSHUSHIA VIFAA VYA UOKOAJI ZA MWAKA 2023

MPANGILIO WA KANUNI

*Kanuni* *Jina*

SEHEMU KWANZA
MASHARTI YA UTANGULIZI

1. Jina.
2. Matumizi.
3. Tafsiri.

SEHEMU YA PILI
UIDHINISHWAJI, VIWANGO VYA UJUZI, UTOAJI WA CHETI, RIPOTI NA KUMBUKUMBU

4. Uidhinishwaji.
5. Viwango vya ujuzi na utoaji wa cheti.
6. Ripoti na kumbukumbu.

SEHEMU YA TATU
UTARATIBU MAALUMU WA UKAGUZI, UTENGENEZAJI, UCHUNGUZI WA KINA, UREKEBISHAJI NA UKARABATI

7. Miongozo ya matengenezo.

8. Uchunguzi wa kina wa kila mwaka na upimaji wa uendeshaji.
9. Mapitio ya vyeti, nk., ya mara kwa mara ndani ya meli.
10. Vitu vya kuchunguzwa na kuangaliwa.
11. Masharti ya ziada ya matengenezo na majaribio.
12. Majaribio ya miaka mitano kuhusiana na utendaji wa vifaa.

SEHEMU YA NNE
MASHARTI YA UIDHINISHWAJI WA WATOA HUDUMA

13. Masharti ya uidhinishwaji wa watoa huduma.
14. Utoaji na utunzaji wa nyaraka za matengenezo.

SEHEMU YA TANO
MASHARTI YA UTHIBITISHAJI WA WAFANYAKAZI

15. Wafanyakazi.
16. Masharti ya uthibitisho.
17. Uhalali wa vyeti na uhuishaji.

SEHEMU YA SITA
MASHARTI YA JUMLA

18. Tathmini na utoaji wa taarifa.
19. Adhabu za jumla.
20. Kushughulikia malalamiko.

SHERIA YA USAFIRI MAJINI,
(SURA YA 165)

# KANUNI

*(Zimetengenezwa chini ya kifungu cha 222)*

KANUNI ZA MASHARTI YA MATENGENEZO, UCHUNGUZI WA KINA, MAJARIBIO YA UENDESHAJI, MAREKEBISHO NA UKARABATI WA BOTI ZA UOKOAJI WA MAISHA, VIFAA VYA UOKOAJI NA VIFAA VYA KUSHUSHIA VIFAA VYA UOKOAJI ZA MWAKA 2023

## SEHEMU YA KWANZA
## MASHARTI YA UTANGULIZI

Jina

1. Kanuni hizi zitajulikana kama Kanuni za Masharti ya Matengenezo, Uchunguzi wa Kina, Majaribio ya Uendeshaji, Marekebisho na Ukarabati wa Boti za Uokoaji wa Maisha, Vifaa Vya Uokoaji na Vifaa vya Kushushia Vifaa vya Uokoaji za Mwaka 2023.

Matumizi

2.-(1) Kanuni hizi zitatumika kwa meli za Tanzania na meli zisizo za Tanzania zikiwa katika maji ya Tanzania hususan katika matengenezo, uchunguzi wa kina, majaribio ya uendeshaji, marekebisho na ukarabati wa-

(a) boti za uokozi wa maisha zikiwemo, boti za uokozi na boti za uokoaji wa haraka; na
(b) vifaa vya kutumbukiza chombo cha uokoaji na zana zinazopakia na zinazotoa nje vifaa vya boti za kuokoa maisha ikijumuisha njia za msingi na za kawaida za kutumbukiza boti za uokoaji wa maisha, boti za uokozi, boti za uokozi wa haraka na kifaa cha kushushia vifaa vya uokoaji.

(2) Bila kuathiri kanuni ndogo ya (1), Kanuni hizi hazitatumika kwa-

(a) meli ya kivita au msaada wa kijeshi;
(b) meli za Jeshi la Ulinzi la Wananchi wa Tanzania;
(c) ndege za baharini za Jeshi la Ulinzi la Wananchi

wa Tanzania; na

(d) meli zinazomilikiwa au kutumiwa na Serikali na kujihusisha na shughuli za kiserikali zisizo za kibiashara.

Tafsiri

3. Katika Kanuni hizi, isipokuwa kama muktadha utahitaji vinginevyo-

"Kanuni za vifaa vya uokozi wa maisha" maana yake ni Kanuni iliyopitishwa na Kamati ya Usalama wa Baharini katika kikao cha 66 (Juni 1996) kwa azimio la Kamati ya Usalama wa Baharini Na. 48(66) au kwa kifupi chake kinachojulikana kama Kanuni ya Kimataifa ya vifaa vya uokozi wa maisha;

"mfumo wa ushushaji usiokuwa na mzigo" maana yake ni mfumo wa njia ya kutoa chombo cha uokozi au boti ya uokozi au boti ya haraka ya uokozi pale inapohitajika kushushwa majini au wakati ambao hakuna mzigo kwenye ndoano;

"mfumo wa ushushaji wenye mzigo" maana yake ni mfumo wa njia ya kutoa chombo cha uokozi au boti ya uokozi au boti ya haraka ya uokozi pale inapohitajika kushushwa majini au wakati ambao kuna mzigo kwenye ndoano;

"Mfumo wa Usimamizi wa Usalama" maana yake ni mfumo ulioandaliwa na kuwekwa katika nyaraka kwa lengo la kuwawezesha watumishi wa kampuni kutekeleza kwa ufanisi Sera ya Usalama na Ulinzi wa Mazingira wa Kampuni;

"mkaguzi" maana yake ni mtu aliyeteuliwa kama mkaguzi chini ya kifungu cha 382 cha Sheria;

"Mkataba wa Usalama" maana yake ni Mkataba wa Kimataifa wa Usalama wa Maisha Baharini wa mwaka 1974 na Itifaki zake za mwaka 1978 na 1988, pamoja na marekebisho yake, au mbadala wake kama utakavyotumika Tanzania;

"mtengenezaji" maana yake ni mtengenezaji wa vifaa halisi au Kampuni yoyote ambayo imechukua majukumu halali na ya kisheria pale ambapo mtengenezaji wa vifaa halisi hayupo au hatengenezi tena vifaa;

"mtoa huduma aliyeidhinishwa" maana yake ni Kampuni

iliyoidhinishwa na Shirika kufanya matengenezo, uchunguzi wa kina, upimaji wa uendeshaji, marekebisho na ukarabati wa boti za uokozi wa maisha na boti za uokozi, vifaa vya kutumbukiza chombo cha uokozi, na utoaji wa zana;

"Notisi ya Usafiri Majini" maana yake ni Notisi iliyoainishwa kama Notisi ya Usafiri Majini na kutolewa na Msajili na inajumuisha rejea ya nyaraka yoyote inayorekebisha au kubadili notisi hiyo;

Sura ya 165

"Sheria" maana yake ni Sheria ya Usafiri Majini;

Sura ya 415

"Shirika" maana yake ni Shirika la Uwakala wa Meli Tanzania lililoanzishwa chini ya kifungu cha 4 cha Sheria ya Wakala wa Meli Tanzania;

"ukarabati" maana yake ni shughuli zozote zinazohitaji kutenganishwa kwa kifaa, au shughuli nyingine zozote nje ya maelekezo ya eneo la matengenezo ya ndani ya meli na matengenezo ya dharura ya vifaa vya uokozi vilivyoandaliwa kulingana na Kanuni za III/36.2, na III/35.3.18 za Mkataba wa Usalama;

"urekebishaji" maana yake ni shughuli ya mara kwa mara inayofanywa na mtengenezaji kwa madhumuni ya kuthibitisha ubora endelevu kwa kipindi kilichoanishwa kulingana na matengenezo sahihi; na

"vifaa" maana yake ni boti za kuokoa maisha na boti za uokoaji, vifaa vya kutumbukiza chombo cha uokozi na zana za uokozi.

## SEHEMU YA PILI
## UIDHINISHWAJI, VIWANGO VYA UJUZI, UTOAJI WA CHETI, RIPOTI NA KUMBUKUMBU

Uidhinishaji

4.-(1) Shirika litahakikisha kwamba, uchunguzi wa kina, upimaji wa uendeshaji na urekebishaji wa vifaa unafanywa na watoa huduma walioidhinishwa kwa mujibu wa kanuni ya 13 wa Kanuni hizi, kanuni ya III/20 ya Mkataba wa Usalama na miongozo iliyotolewa na Shirika kupitia Notisi ya Usafiri Majini katika uzingatiaji wa vifaa vya baharini na viwango vilivyoidhinishwa.

(2) Masharti ya kanuni ya 13 ya Kanuni hizi, yatatumika vilevile kwa watengenezaji wanapokuwa

wanafanya kazi kama watoa huduma walioidhinishwa.

Viwango vya ujuzi na utoaji wa vyeti

5.-(1) Ukaguzi wa kila wiki na kila mwezi na matengenezo ya mara kwa mara yatafanywa na watoa huduma walioidhinishwa au wafanyakazi wa ndani ya meli chini ya maelekezo ya afisa mwandamizi wa meli kama ilivyoainishwa katika kitabu cha mwongozo wa matengezo ya vifaa husika.

(2) Uchunguzi wa kina namajaribio ya uendeshajiwa kila mwaka kama ilivyoainishwa chini ya kanuni ya 8, utafanywa na wafanyakazi walioidhinishwa wa mtengenezaji au mtoa huduma kwa mujibu wa kanuni za 13 na 14.

(3) Mtoa huduma aliyerejewa chini ya kanuni ndogo ya (1), anaweza kuwa opareta wa meli ilimradi ameidhinishwa kwa mujibu wa kanuni za 4, 13 na 14.

(4) Uchunguzi wa kina, urekebishaji, upimaji wa uendeshaji na ukarabati wa miaka mitano utafanywa na watu walioidhinishwa wa mtengenezaji au mtoa huduma aliyeidhinishwa kwa mujibu wa kanuni za 13 na 15.

(5) Uchunguzi wa kina au urekebishaji na upimaji wa uendeshaji unaorejewa chini ya kanuni ndogo ya (4), utafanyika mbele ya mpimaji.

Ripoti na kumbukumbu

6.-(1) Ripoti na orodha za ukaguzi zitaandaliwa na kusainiwa na mtu atakayefanya ukaguzi na matengenezo, na kusainiwa pia na mwakilishi wa Kampuni au nahodha wa meli.

(2) Kumbukumbu za matengenezo, uchunguzi wa kina, upimaji wa uendeshaji, urekebishaji na ukarabati zitahuishwa na kuwekwa kwenye meli kwa kipindi chote cha utendaji kazi wa kifaa.

(3) Pale ambapo uchunguzi wa kina, upimaji wa uendeshaji, urekebishaji na ukarabati umekamilika, mtengenezaji au mtoa huduma aliyeidhinishwa aliyefanya kazi husika atatoa mara moja taarifa inayothibitisha kwamba mipangilio ya boti ya uokozi wa maisha bado inafaa kutumika.

(4) Taarifa iliyorejewa chini ya kanuni ndogo ya (3), itaambatishwa na nakala ya hati halisi za uthibitisho na

idhini.

## SEHEMU YA TATU
## UTARATIBU MAALUMU WA UKAGUZI, UTENGENEZAJI, UCHUNGUZI WA KINA, UREKEBISHAJI NA UKARABATI

Miongozo ya matengenezo

7.-(1) Ukaguzi wowote, matengenezo, uchunguzi wa kina, upimaji wa uendeshaji, urekebishaji na ukarabati utafanywa kulingana na miongozo ya matengenezo na nyaraka zinazohusiana na utunzaji wa kiufundi zilizoandaliwa na mtengenezaji.

(2) Mmiliki na nahodha wa meli atahakikisha kwamba, seti kamili ya miongozo ya matengenezo inayotumika na nyaraka za kitaalam zinazohusiana na utunzaji zinapatikana kwenye meli.

(3) Miongozo ya matengenezo na nyaraka za kiufundi zinazohusiana zitajumuisha vifaa kama vilivyoorodheshwa chini ya kanuni ya 10 kama kiwango cha chini na kuhuishwa na Kampuni kwa kuzingatia taarifa halisi zinazotolewa na mtengenezaji.

Uchunguzi wa kina wa kila mwaka na upimaji wa uendeshaji

8. Orodha ya vifaa vya ukaguzi wa kila wiki na kila mwezi chini ya Kanuni za III/20.6 na III/20.7 za Mkataba wa Usalama zitakuwa sehemu ya uchunguzi wa wa kina wa kwanza wa kila mwaka.

Mapitio ya vyeti, nk., ya mara kwa mara ndani ya meli

9. Kumbukumbu za ukaguzi na matengenezo ya mara kwa mara ndani ya meli zitaandaliwa na wafanyakazi wa meli na vyeti vinavyotumika kwa ajili ya vifaa vitafanyiwa mapitio kwa mujibu wa masharti yanayotumika katika Mfumo wa Usimamizi wa Usalama.

Vitu vya kuchunguzwa na kuangaliwa

10.-(1) Vitu vifuatavyo vitachunguzwa kwa kina na kuangaliwa kwa ajili ya kujiridhisha na hali yake na uendeshaji katika boti za kuokoa maisha ikiwa ni pamoja na boti za kuokoa maisha zinazoserereka, boti za uokozi na boti za uokozi wa haraka:

(a) hali ya muundo wa boti ikijumuisha vifaa vilivyofungwa na ambavyo havijafungwa, ikiwa ni pamoja na uchunguzi wa kuona mipaka ya nje

ya eneo la wazi, kadiri inavyowezekana;

(b) injini na mfumo ya uzungushaji;

(c) mfumo wa kunyunyizia, endapo umewekwa;

(d) mfumo wa usambazaji hewa, endapo umewekwa;

(e) mfumo wa uendeshaji;

(f) mfumo wa usambazaji umeme;

(g) mfumo wa utoaji maji;

(h) mipangilio ya vizuizi vya meli; na

(i) mfumo wa uwekaji boti ya uokozi katika usawa stahiki.

(2) Yafuatayo yatachunguzwa kwa kina ili kubaini hali na uendeshaji wa winchi breki inapokuwa na boti tupu au mzigo sawa na huo katika gia ya kutolea boti za kuokoa maisha ikiwa ni pamoja na boti za uokozi wa maisha zinazoserereka, boti za uokozi, boti za uokoaji wa haraka:

(a) uendeshaji wa vifaa vya kuwezesha gia ya kutolea;

(b) kucheza kunakozidi ikijumuisha hali yake ya uvumilivu;

(c) mfumo wa hydrostatiki, endapo umewekwa;

(d) kebo za kuzuia na kuruhusu; na

(e) vifungia ndoano.

(3) Vifaa vifuatavyo vitachunguzwa kwa kina na kuangaliwa kwa ajili ya kujiridhisha na hali yake na uendeshaji katika vifaa vya kutumbukiza boti za kuokoa maisha ikiwa ni pamoja na boti za uokozi wa maisha zinazoserereka, boti za uokozi, boti za uokoaji wa haraka:

(a) daviti au miundo ya vifaa vingine vya kushushia, hasa kuhususiana na kutu, kupishana, kubondeka na kucheza kunakozidi;

(b) waya, mfuo, uwezekano wa uharibifu kama vile kuharibika kwa kamba na kutu; na

(c) ulainishaji wa waya, mfuo na sehemu zinazozunguka;

(d) pale inapowezekana-

(i) utendaji kazi wa swichi za kikomo;

(ii) mifumo ya nishati iliyohifa dhiwa;

(iii) mfumo wa kimiminika; na

(iv) winchi;

(e) kukagua mfumo wa breki kwa mujibu wa mwongozo wa kitabu;
(f) kubadilisha pedi za breki, pale inapobidi;
(g) msingi wa winchi; na
(h) pale inapowezekana-
  (i) mfumo wa udhibi kwa rimoti; na
  (ii) mfumo wa usambazaji nishati.

Masharti ya ziada ya matengenezo na majaribio

11.-(1) Uangalifu mkubwa utachukuliwa wakati wa kufanya shughuli zote za ukaguzi na matengenezo kwenye kifaa cha kushushia kwa kuwa mpangilio na matengenezo ya kifaa cha kushushia ni shughuli muhimu kuhusiana na kudumisha utendaji kazi salama wa boti za kuokoa maisha ikiwa ni pamoja na boti za uokozi wa maisha zinazoserereka, boti za uokozi, boti za uokoaji wa haraka na boti zinazoteremshwa kwa kutumia daviti.

(2) Matengenezo au marekebisho ya kifaa cha kushushia hayatafanywa wakati ndoano ikiwa na mzigo.

(3) Upimaji wa uendeshaji wa boti zinazoshushwa kwa kifaa cha daviti na boti za uokozi kwa mfumo wa ushushaji wenye mzigo utafanywa kama ifuatavyo:

(a) weka boti kwa kiasi fulani ndani ya maji ili kwamba uzito wa boti kwa kiasi kikubwa kuwa umeshikwa na vishikizo na mfumo wa hydrostatiki, endapo umefungwa, ukiwa haujaanzishwa;
(b) endesha kifaa cha ushushaji chenye mzigo;
(c) rekebisha kifaa cha ushushaji chenye mzigo; na
(d) kuchunguza gia ya kutoa na kufunga ndoano ili kuhakikisha kuwa ndoano imewekwa upya na hakuna uharibifu wowote uliotokea.

(4) Upimaji wa uendeshaji wa boti za kuokoa maisha zilizozinduliwa na daviti na boti za uokoaji kutolewa kwenye mzigo utafanywa kama ifuatavyo:

(a) weka boti ili isiweze kupita maji kabisa;
(b) endesha kifaa cha kushushia kisichokuwa na mzigo;
(c) rekebisha kifaa cha kushushia kisichokuwa na mzigo; na

(d) rejesha boti mahali palipowekwa na kujiandaa kwa utayari wa kufanya kazi.

(5) Wakati wa upimaji, kabla ya kuinua, kifaa cha kushushia itaangaliwa ili kuhakikisha kuwa imewekwa kikamilifu na ipasavyo na ugeuzaji wa boti utafanywa bila mtu yeyote kuwa ndani.

(6) Upimaji wa uendeshaji wa boti za kuokoa maisha zinazoserereka kwa mfumo wa kuiachia itafanywa kama ifuatavyo:

(a) tumia maandalizi ya upimaji bila kuiachia boti ya kuokoa maisha, kama inavyohitajika na aya ya 4.7.6.4 ya Kanuni za Kimataifa za Vifaa vya Uokozi wa Maisha, kama ilivyobainishwa katika miongozo ya uendeshaji kutoka kwa mtengenezaji;

(b) iwapo atahitajika kuwa ndani ya meli, hakikisha kwamba mwendeshaji ameketi vizuri na ameshikiliwa vizuri katika eneo la kiti ambapo mfumo wa ushushaji unapaswa kuendeshwa;

(c) endesha mfumo wa ushushaji ili kuachia boti ya uokoaji wa maisha;

(d) rekebisha boti ya kuokoa maisha katika mpangilio uliowekwa;

(e) rudia taratibu zilizorejewa katika aya (b) hadi (d), kwa kutumia utaratibu mbadala wa mfumo wa kuachia, endapo unatumika;

(f) ondoa mipangilio ya uendeshaji kwa kujaribu bila kuiachia boti ya kuokoa maisha, kama inavyohitajika katika aya ya 4.7.6.4 ya Kanuni za Kimataifa za Vifaa vya Uokozi wa Maisha; na

(g) thibitisha kuwa boti ya kuokoa maisha iko tayari kuachia mipangilio iliyowekwa.

(7) Upimaji wa uendeshaji wa kifaa cha uokoaji kinachoshushwa kwa kifaa cha ushushaji cha daviti utazingatia yafuatayo:

(a) toa kwa mkono ndoano yenye mzigo wa kilo 150 kwenye ndoano;

(b) achia ndoano moja kwa moja yenye uzito wa kilo 200 kwenye ndoano inaposhushwa chini; na

(c) chunguza ndoano ya kuachia na vifungia ndoano

ili kuhakikisha kuwa ndoano imewekwa kikamilifu kabisa na hakuna uharibifu uliotokea.

(8) Pale ambapo kifaa cha uokoaji kinatumiwa kwa jaribio badala ya uzani wa dumi, kitendakazi cha kuachia kiotomatiki kitaachia kifaa cha uokoaji pale ambapo kifaa hicho kimefika kwenye maji.

(9) Kwa winchi za vifaa vya kushushia boti za kuokoa maisha ikiwa ni pamoja na boti za kuokoa maisha zinazoserereka, boti za uokozi na boti za uokozi wa haraka, majaribio ya kila mwaka ya uendeshaji yatafanywa kwa kushusha chomboau boti tupu au mzigo sawa na huo.

(10) Pale ambapo chombo kimefikia kiwango chake cha juu cha kasi ya ushushaji na kabla ya chombo kuingia ndani ya maji, breki itawekwa kwa ghafla na kufuatana na majaribio chini ya kanuni ndogo ya (9), sehemu za muundo zilizosisitizwa zitakaguliwa upya pale ambapo muundo unaruhusu kukaguliwa upya.

Majaribio ya miaka mitano kuhusiana na utendaji wa vifaa

12.-(1) Majaribio ya miaka mitano ya uendeshaji wa winchi za vifaa vya uokoaji yatafanywa na mzigo wa uthibitisho sawa na mara 1.1 ya uzito wa kifaa cha kuokoa au boti ya uokoaji na ukamilishaji wake wa watu na vifaa na wakati mzigo wa uthibitisho umefika kiwango cha juu cha kasi ya ushushaji, breki itatumika kwa ghafla.

(2) Kufuatia majaribio yaliyorejewa chini ya kanuni ndogo ya (1), sehemu za kimuundo zilizosisitizwa zitakaguliwa tena pale ambapo muundo unaruhusu kukaguliwa upya.

(3) Majaribio ya uendeshaji na urekebishaji katika vipindi vya miaka mitano ya kifaa cha kushushia boti za kuokoa maisha ikiwa ni pamoja na boti za kuokoa maisha zinazoserereka, boti za uokoaji, boti za uokoaji wa haraka na vifaa vya uokoaji yatajumuisha-

(a) kuvunjwa kwa vifaa vya kutoa ndoano;
(b) uchunguzi wa uvumilivu na mahitaji ya muundo;
(c) marekebisho ya mfumo wa kifaa cha kushushia vifaa vya uokoaji baada ya kufungwa;
(d) majaribio ya uendeshaji kama yanavyotumika, lakini yenye mzigo unaolingana na mara 1.1 ya

uzito wa boti ya kuokoa maisha na ukamilishaji wake kamili wa watu na vifaa;

(e) uchunguzi wa kasoro na nyufa katika sehemu muhimu; na

(f) urekebishaji mwingine wowote ukihitajika utafanywa kwa mujibu wa kanuni ya 5(3).

## SEHEMU YA NNE
## MASHARTI YA UIDHINISHAJI WA WATOA HUDUMA

Masharti ya uidhinishwaji wa watoa huduma

13.-(1) Uidhinishaji wa watoa huduma utajumuisha-

(a) ajira na nyaraka za wafanyakazi waliothibitishwa kwa mujibu wa viwango vinavyotambulika vya kitaifa, kimataifa au sekta husika, au mpango ulioanzishwa na mtengenezaji wa uthibitishaji na kwa vyovyote vile, programu ya uthibitishaji itazingatia kanuni ya 16 kwa huduma inayopaswa kutolewa kwa kila aina ya kifaa;

(b) upatikanaji wa zana za kutosha, na hasa zana maalum zilizoainishwa katika mwongozo wa mtengenezaji, ikiwa ni pamoja na zana zinazobebeka kama zinahitajika kwa kazi itakayofanywa kwenye meli;

(c) upatikanaji wa vipuri na vifaa sahihi kama ilivyoainishwa kwa ajili ya matengenezo na ukarabati;

(d) upatikanaji wa miongozo ya mtengenezaji kwa ajili ya kazi ya ukarabati inayohusisha kufunguliwa au marekebisho ya mfumo wa ushushaji wenye mizigo na winchi za daviti; na

(e) mfumo wa ubora uliorekodiwa na kuthibitishwa, ambao unajumuisha angalau yafuatayo:

(i) kanuni za maadili kwa wafanyakazi wanaohusika katika shughuli husika;

(ii) matengenezo na urekebishaji wa zana za kupimia na vipimo;

(iii) mipango ya mafunzo na vyeti kwa wafanyakazi;

(iv) usimamizi na uhakiki ili kuhakikisha uzingatiaji wa taratibu za uendeshaji;

(v) kurekodi na kuripoti habari;

(vi) usimamizi wa ubora wa tanzu na mawakala;

(vii) maandalizi ya kazi; na

(viii) ikiwa kutakuwa na mazingira ya kufutwa kwa cheti kilichotolewa kwa mfanyakazi yeyote, notisi ya kuonyesha sababu atakayopewa;

(ix) mapitio ya mara kwa mara ya taratibu za kufanya kazi, malalamiko, hatua za kurekebisha na utoaji, utunzaji na udhibiti wa nyaraka.

(2) Mfumo wa ubora uliorekodiwa unaozingatia toleo la kisasa zaidi la mfululizo wa ISO 9000 na unaojumuisha masuala yaliyoainishwa chini ya kanuni ndogo ya (1) utachukuliwa kuwa unakubalika.

(3) Shirika litahakikisha kwamba taarifa zinazowahusu watoa huduma walioidhinishwa zinapatikana kupitia Notisi ya Usafiri Majini.

(4) Pale ambapo mtengenezaji ameacha biashara au kutoa usaidizi wa kiufundi, Shirika linaweza kuwaidhinisha watoa huduma wa kifaa kwa kuzingatia idhini ya awali ya kifaa au uzoefu wa muda mrefu na utaalam utakaoonyeshwa kama mtoa huduma aliyeidhinishwa.

Utoaji na utunzaji wa nyaraka za matengenezo

14.-(1) Baada ya kufanikiwa kwa ukaguzi wa awali wa mtoa huduma, hati ya idhini itatolewa na Shirika inayofafanua wigo wa huduma zinazotolewa na tarehe ya kuisha itaandikwa kwa uwazi kwenye hati.

(2) Shirika litahakikisha kwamba kazi inaendelea, kwa kufanya ukaguzi wa mara kwa mara kwa mujibu wa masharti haya, na itafuta idhini ya watoa huduma wasiozingatia.

(3) Shirika linaweza kukubali au kutambua watoa huduma walioidhinishwa na mamlaka ya nchi nyingine au na Mashirika yao Yanayotambuliwa.

## SEHEMU YA TANO
## MASHARTI YA UTHIBITISHAJI WA WAFANYAKAZI

Wafanyakazi

15. Wafanyakazi kama ilivyoainishwa katika kanuni ya 5, watathibitishwa na mtengenezaji au mtoa huduma aliyeidhinishwa kwa kila utengenezaji na aina ya vifaa vitakavyofanyiwa kazi kwa mujibu wa masharti ya kanuni hii.

Masharti ya udhibitisho

16.-(1) Udhibitisho wa awali utatolewa kwa wafanyakazi waliohitimu elimu, mafunzo na tathmini ya uwezo.

(2) Elimu inayorejewa katika kanuni ndogo ya (1) itashughulikia-

(a) sheria na kanuni husika, ikijumuisha mikataba ya kimataifa;
(b) ubunifu na ujenzi wa boti za kuokoa maisha zikiwemo boti za kuokoa maisha zinazoserereka, boti za uokozi na boti za uokozi wa haraka, ikijumuisha vifaa vya kushushia vyenye mizigo na vifaa vya uokoaji;
(c) sababu za ajali za boti za uokoaji;
(d) elimu na mafunzo kwa vitendo katika taratibu zilizoainishwa chini ya Sehemu ya Tatu ya Kanuni hizi yanayohitaji uthibitisho;
(e) taratibu za kina za uchunguzi wa kina, upimaji wa uendeshaji, urekebishaji na ukarabati wa boti za kuokoa maisha zikiwemo boti za kuokoa maisha zinazoserereka, boti za uokozi na boti za uokozi wa haraka, vifaa vya kushushia na vifaa vya kushushia vyenye mizigo, kama inavyotumika;
(f) taratibu za kutoa ripoti ya utumishi na taarifa ya kufaa kwa madhumuni kulingana na kanuni ya 6(3); na
(g) masuala ya kazi, afya na usalama wakati wa kufanya kazi melini.

(3) Mafunzo yatajumuisha mafunzo ya kiufundi kwa vitendo juu ya mbinu za uchunguzi wa kina, upimaji wa uendeshaji, matengenezo, ukarabati na urekebishaji kwa kutumia vifaa ambavyo wafanyakazi wanatakiwa kuthibitishwa.

(4) Mafunzo ya kiufundi chini ya kanuni ndogo ya (3) yatajumuisha kutenganisha, kuunganisha upya, uendeshaji

sahihi na marekebisho ya vifaa.

(5) Mafunzo ya darasani yatakamilishwa na mafunzo ya vitendo katika uendeshaji ambao uthibitisho unahitajika, chini ya usimamizi wa mtu aliyethibitisha.

(6) Kabla ya utoaji wa uthibitisho, tathmini ya uwezo itakamilika kwa njia ya kuridhisha, kwa kutumia vifaa ambavyo wafanyakazi wanatakiwa kuthibitishwa.

Uhalali wa vyeti na uhuishaji

17.-(1) Baada ya kukamilika kwa mafunzo na tathmini ya uwezo, cheti kitatolewa kinachofafanua kiwango cha sifa na upeo wa uthibitisho.

(2) Tarehe ya kuisha kwa cheti kilichorejewa chini ya kanuni ndogo ya (1), itaandikwa kwa uwazi na itakuwa kwa muda wa miaka mitatu kuanzia tarehe ya kutolewa.

(3) Uhalali wa cheti chochote unaweza kusitishwa iwapo kuna upungufu wowote katika utendaji kazi na kutolewa upya baada ya tathmini ya uwezo ya ziada.

(4) Tathmini ya uwezo itafanywa ili kufanya upya uthibitishaji na katika hali ambapo mafunzo ya kujiendeleza yataonekana kuwa muhimu tathmini zaidi itafanywa baada ya kukamilika.

## SEHEMU YA SITA
## MASHARTI YA JUMLA

Tathmini na kuwasilisha taarifa

18.-(1) Msajili atapaswa-

(a) kufanya tathmini ya masharti ya udhibiti yaliyomo katika Kanuni hizi;

(b) kuandaa ripoti inayoeleza hitimisho kwa tathmini; na

(c) kuwasilisha taarifa kwa Waziri.

(2) Taarifa ya kwanza chini ya kanuni hii itachapishwa kabla ya mwaka wa tano wa tarehe ambayo Kanuni hizi zitaanza kutumika.

(3) Taarifa zinazofuata zitachapishwa kwa vipindi visivyozidi miaka mitano.

(4) Taarifa iliyotayarishwa na kuwasilishwa chini ya kanuni hii, itapaswa-

(a) kuweka malengo yanayokusudiwa kufikiwa na masharti ya udhibiti yanayorejewa katika kanuni

ndogo ya (1)(a);

(b) kutathmini kiwango ambacho malengo hayo yanafikiwa;

(c) kutathmini kama malengo hayo bado yanafaa; na

(d) pale ambapo malengo yataonekana kuwa yanafaa, kutathmini kiwango ambacho yanaweza kufikiwa kwa njia nyingine ambayo inahusisha masharti mepesi ya udhibiti.

Adhabu za jumla

19. Mtu anayekiuka masharti ya Kanuni hizi anatenda kosa na endapo atatiwa hatiani atawajibika kulipa faini isiyopungua dola za Marekani elfu moja au kiwango kinacholingana katika shilingi za Kitanzania au kifungo kwa kipindi kisichozidi miezi sita au vyote kwa pamoja.

Kushughulikia malalamiko TS. Na. 338 la 2018

20. Mtu ambaye hajaridhika na uamuzi uliotolewa chini ya Kanuni hizi anaweza kuwasilisha maombi ya mapitio kwa Shirika kwa mapitio kwa mujibu wa Kanuni za Ushughulikiaji wa Malalamiko za Wakala wa Meli Tanzania.

Dodoma,
28 Juni, 2023

MAKAME M. MBARAWA,
*Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi*